

UTAJIRI NA KUOKOKA

Ndugu zangu; imeandikwa “Kwa maana mnajua neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba **ingawa alikuwa tajiri, kwa ajili yenu alikubali kuwa maskini, ili kwa umaskini Wake ninyi mpate kuwa matajiri**” (2korinth.8:9). Yaani kama vile ambavyo “Kristo alitukomboza kutoka katika laana ya sheria kwa kufanyika laana kwa ajili yetu, kwa maana imeandikwa, ‘Amelaaniwa yeye aangikwaye juu ya mti’...ili kwa imani tupate kupokea ile ahadi ya Roho (wagalatia.3:13-14). **Tatizo watu wengi hatusomi biblia na tunaishia kusikia mistari kutoka kwa watu kiasi kwamba wengi mnaogopa kua matajiri. Na ninahasira ya kimungu na huu upotovo, ni lazima sisi tuwe mwanga ili wengine watamani.**

Alieokoka anakua mtoto wa Mungu. Yaani anakua mtoto wa Mfalme. (wagalatia.3:26-29). Kama umeokoka...Katika ulimwengu wa kiroho wewe ni “prince” na katika ulimwengu wa kimwili Mungu anakuona wewe ni mfalme. Ndio maana Yesu anaitwa “Mfalme wa wafalme”. **Sasa Je, mtoto wa mfalme anaweza kuwa maskini?** Basi ukiona mtoto wa Mungu ni maskini lazima huyo mtoto anamatatizo. Lakini pia kwakuwa Mungu anaona mwanzo na mwisho, **wengine akili zao hazipo tayari** kiasi kwamba hawaruhusiwi kua na utajiri ili wasije wakamkufuru Mungu na hatimae kupoteza wokovu.

Kwa mfano Yesu alisema “Hakuna mtu ye yote awezaye kuwatumikia mabwana wawili, kwa kuwa ama atamchukia huyu na kumpenda yule mwingine” na mbele kidogo akasema “Ninyi hamwezi kumtumikia Mungu na mali”. Na siku nyingine Yesu alisema “ni rahisi zaidi kwa ngamia kupita kwenye tundu la sindano kuliko mtu tajiri kuingia katika Ufalme wa Mungu”. Petro akamwuliza “Ni nani basi awezaye **kuokoka?**” Lakini Yesu akawatazama, akawaambia, “**Kwa mwanadamu jambo hili haliwezekani, lakini kwa Mungu mambo yote yanawezekana**” (Mathayo.19:16-26).

Sasa kama Yesu anasema “kwa Mungu mambo yote yanawezaka”... je, Inawezekanaje? Ndugu zangu, Yesu anajibu mwenyewe kwa kusema “Msijiwekee hazina duniani, mahali ambapo **nondo na kutu** huharibu, **nao wevi huvunja na kuiba**. Lakini jiwekeeni hazina mbinguni, mahali ambapo nondo na kutu haviharibu, wala wevi hawavunji na kuiba. **Kwa sababu mahali akiba yako ilipo, hapo ndipo pia moyo wako utakapokuwa**” (mathayo.5:24, 6:19-21)

Je tunawekaje akiba mbinguni? Akiba huwekwa mbinguni kwa kutoa zaka na sadaka (kujitolea). Katika lugha ya kibinadamu, zaka ni kodi (10%) na sadaka ni “investments”. Sasa hapa wengi hawajui hapa ... kwa mfano zaka (kodi) mtu anatoa 10,000tsh lakini anawekeza(sadaka) 100tsh. **Sasa wote mnajua kua ukiwekeza kidogo...utazidishiwa kidogo.** Na ndio maana hakuna maandeleo kwa walio wengi. Zaka ni kwa ajili ya kufungua madirisha (orpotunities) mbalimbali za biashara zako na sadaka ni ndio uwekezaji wenyewe. Vilevile zaka ni kiashiria cha wewe kuthibitisha kua ulichopewa ni cha Mungu na unadhihirisha kwa kumrudishia 10% ya alichokupa. Na sadaka si lazima iende kanisani. Kutoa misaada pia ni kutoa sadaka (soma Malaki.3:6-12)

Mungu amewaonya waziwazi wale wanaopata utajiri na kuweka hazina yao duniani kwa kusema “sikilizeni, ninyi matajiri, lieni na kuomboleza kwa ajili ya hali mbaya sana inayowajia. Utajiri wenu umeoza na mavazi yenu **yameliwa na nondo**. Dhahabu yenu na fedha yenu **vimeliwa na kutu**. **Kutu** yake itashuhudia dhidi yenu nayo itaila miili yenu kama vile moto”. Tena anasema “Angalieni! Ule ujira wa vibarua waliolima mashamba yenu mliouzuia kwa hila unapiga kelele dhidi yenu na vilio vya wavunaji vimefika masikioni mwa Bwana wa majeshi” (Yakobo.5:1-6)

Lakini kwa wanaopata utajiri kwa jina la Yesu... Roho Mtakatifu kwa mkono wa Paulo anasema “waagize wale ambao ni matajiri wa ulimwengu huu waache kujivuna, wala wasiweke tumaini lao katika mali ambayo si ya hakika, bali waweke tumaini lao katika Mungu ambaye **hutupatia vitu vyote** kwa wingi ili tuvifurahie. Waagize watende mema, wawe matajiri katika matendo mema, pia wawe wakarimu na walio tayari kushiriki mali zao na wengine. Kwa njia hii watajiwekea hazina kama msingi kwa ajili ya wakati ujao na hivyo watajiipatia uzima, yaani, ule uzima ambao ni wa kweli”. (1timoth.6:17-19)

Mpagani husema moyoni mwake “**pesa kwanza Mungu baadae**”. Mtu kama huyu shetani anamchukua na kumtajirisha sana na kumfanya mtego kiasi kwamba hata Mungu akimuokoa afisilisike kabisa ili uwe mfano mbaya na hatimae wengi wakatae kupokea wokovu (kuokoka). Na kwasababu Mungu hafanyi Mambo yake kwa kubahatisha...ataangalia **cost/benefit ratio**. Akiona itafanya wengi wakatae wokovu, basi humuacha huyo mtu afe bila wokovu. Hao ni waabudu sanamu (pesa) na ndio wale Yesu alisema “ni rahisi zaidi kwa ngamia kupita kwenye tundu la sindano kuliko mtu tajiri kuingia katika Ufalme wa Mungu”. *[kwa wanaojiuliza “KUOKOKA NI NINI?” subirini next article inakuja]*

Kwahiyo ni jambo jema sana kwa sisi vijana kuacha uvuguvugu mapema. Yaani kule kumwamini Yesu kua Mwokozi wetu lakini hatutaki awe **Bwana** wetu. Tumpokee Yesu kwanza ili utajiri wetu uwe ni kwa Jina la Yesu. Imeandikwa “**utafuteni kwanza Ufalme wa Mungu na haki yake na haya yote mtaongezewa.**” Hapo kwenye “haya yote” na Utajiri upo ndani yake. Kwa maana “Unyenyekevu na kumcha BWANA huleta **utajiri, heshima na uzima**”. (Mathayo.6:33, Mithali.22:4)